**HOTUBA YA MWENYEKITI WA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI MHE. JAJI (R) (MST.) SEMISTOCLES S. KAIJAGE KATIKA UFUNGUZI WA KIKAO CHA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI NA WAHARIRI WA VYOMBO VYA HABARI KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA KIMATAIFA WA MWL. J. K. NYERERE**

**18 AGOSTI, 2020**

- **Mhe. Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi,**
- **Waheshimiwa Wajumbe wa Tume,**
- **Wahariri wa Vyombo vya Habari,**
- **Mkurugenzi wa Uchaguzi,**
- **Watendaji wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi,**
- **Wanahabari,**
- **Mabibi na Mabwana.**

*Bwana Asifiwe,*
*Tumsifu Yesu Kristo,*
*Assalam Aleykum.*

Awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na kutuwezesha kukutana kwa mara nyingine siku ya leo kwa ajili ya kikao hiki muhimu. Kukutana kwetu hapa ni muhimu kwa mustakabali wa nchi yetu hasa katika kipindi hiki tunapoelekea katika Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2020.

Kipekee, niwashukuru ndugu Wahariri kwa kuitikia wito na kuhudhuria kikao hiki ambacho kinakusudiwa, pamoja na mambo mengine, kutoa taarifa ya maandalizi mbalimbali ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Hatua hii pia inalenga kuwashirikisha kwenye hatua mbalimbali za michakato ya uchaguzi kwa kadri inavyowezekana. **Karibuni sana**.

**Ndugu Wahariri wa vyombo vya habari;**

Nitumie nafasi hii kuwashukuru kwa kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake na kuiwezesha kuwa karibu na Wadau wa Uchaguzi kwa njia ya taarifa na habari mnazozitoa kwa wakati. Hali kadhalika, kuiwezesha Tume kutumia vyombo vyenu kwa ajili ya elimu ya mpiga kura na kufafanua hoja mbalimbali kutoka kwa wadau.

Mathalan, baadhi ya magazeti yametupa kurasa zake ili kuchapisha makala za kuelimisha umma kuhusu Tume na majukumu yake. Redio na Runinga zimetoa nafasi kwa Tume kushiriki vipindi mbalimbali vyenye kulenga kutoa elimu kwa wapiga kura. Ni dhahiri kwamba bila ushirikiano huo Tume isingeweza kufanikisha jambo hilo.

**Ndugu Wahariri wa vyombo vya Habari;**

Kwa niaba ya Tume napenda kuwashukuru waandishi wa habari, ambao ndio wanaofanya kazi kwa karibu zaidi nasi, na kila tunapowahitaji hawajawahi kusita kushirikiana nasi. Tumewaona daima wakitoa kipaumbele kwa shughuli na taarifa za Tume. **Asanteni sana**.

**Ndugu Wahariri wa vyombo wa Habari;**
Tume inavitambua Vyombo vya Habari kwa namna mbili. Mosi, kama daraja linalounganisha Tume na wadau kwa njia ya mawasiliano na pili, kama mojawapo ya Wadau muhimu wa Uchaguzi. Hivyo, kwa siku ya leo mko hapa kama Wadau muhimu wa uchaguzi ili tuweze kuwafahamisha hatua mbalimbali za maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

Napenda kuwafahamisha kuwa, hadi sasa Tume imefanya maandalizi mbalimbali ya Uchaguzi Mkuu. Hata hivyo, ili zoezi hili lifanikiwe, kwa kiwango kikubwa linategemea sana ushirikiano wenu Wahariri na Waandishi wa Habari, katika kutoa taarifa na kuwaelimisha Wananchi juu ya umuhimu wa zoezi hili.

Katika muktadha huo, Tume inaamini kuwa mkipata uelewa mzuri wa michakato ya uchaguzi basi itakuwa rahisi kwenu kuwaelimisha na kuwahamasisha wananchi kupitia vyombo vyenu vya habari ili kushiriki kikamilifu katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

Dhamira hiyo ndiyo iliyoisukuma Tume kuandaa kikao cha pamoja ili kupeana taarifa na kufahamishana kuhusu maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu. Vilevile, kupitia kikao hiki tutapata nafasi ya kubadilishana na kupeana uzoefu kuhusu utekelezaji wa shughuli za uchaguzi.

**Ndugu Wahariri wa vyombo wa Habari**;

Katika maandalizi ya Uchaguzi Mkuu, Tume imekamilisha uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ambao ulifanyika mara mbili kama inavyoelekezwa katika kifungu cha 15 (5) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 21 (5) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292.

Uboreshaji wa Daftari ulianza tarehe 18 Julai, 2019 na kukamilika 20 Juni, 2020. Katika kipindi hicho, awamu mbili za uboreshaji wa daftari zilifanyika halikadhalika uwekaji wazi wa daftari la awali.

Katika awamu zote mbili, uboreshaji ulifanyika katika vituo **37,814** vya kuandikisha wapiga kura**. K**atika zoezi hilo Jumla ya Wapiga Kura wapya **7,326,552** waliandikishwa sawa na asilimia **31.63** ya Wapiga Kura **23,161,440** walioandikishwa mwaka 2015. Aidha, Jumla ya Wapiga Kura **3,548,846** waliboresha taarifa zao na Wapiga Kura **30,487** waliondolewa kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kutokana na kukosa sifa kwa mujibu wa sheria. Baada ya kuwaondoa Wapiga Kura ambao taarifa zao zimejirudia, kwa hivi sasa Daftari lina jumla ya Wapiga Kura wapatao **29,188,347.**

Kutokana na idadi hiyo ya wapiga kura, katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu kutakuwa na vituo **80,155** vya kupigia kura na kila kituo kimoja kitakuwa na Wapiga Kura wasiozidi **500**.

**Ndugu wahariri wa vyombo Habari;**

Katika maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu, hakukuwa na marekebisho katika Sheria za Uchaguzi. Hata hivyo, Tume imefanya maboresho ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 na Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020. Hali kadhalika, imekamilisha Maelekezo ya Uchaguzi kwa ajili ya wadau mbalimbali na Watendaji wa Uchaguzi.

**Ndugu Wahariri wa vyombo vya Habari;**

Ili kuleta uwazi katika mchakato mzima wa Uchaguzi Mkuu, Tume imekuwa ikiwashirikisha wadau wa uchaguzi, mkiwemo ninyi, katika hatua mbalimbali za mchakato wa Uchaguzi.

Mathalan, kabla ya kuanza zoezi la uboreshaji, Tume ilikutana na Wahariri wa Vyombo vya Habari tarehe 16 Juni, 2019 katika Ukumbi huu na kupokea maoni yenu.

Maeneo mengine ya ushirikishwaji wa wadau yalihusu nyaraka muhimu za zoezi la uboreshaji ambapo Tume ilivipatia vyama vya siasa nyaraka mbalimbali kama vile orodha ya vituo vya uandikishaji vya nchi nzima, Kanuni za Uboreshaji na ratiba za mazoezi mbalimbali.

Aidha, Tume imekuwa na utaratibu wa kukutana na wadau mbalimbali ikiwemo Vyombo vya Habari, Vyama vya Siasa, Viongozi wa Dini na Makundi Maalum kama vile Wanawake, Vijana, Watu Wenye Ulemavu, Asasi za Kiraia na katika maeneo mengine Wazee wa Kimila. Mikutano hii ilifanyika pia katika kila mkoa kabla ya kuanza kwa zoezi la uandikishaji wa wapiga kura. Katika mikutano hiyo, Tume ilinufaika kwa mawazo na michango mingi iliyosaidia katika utekelezaji wa shughuli za maandalizi ya Uchaguzi Mkuu.

**Ndugu Wahariri wa vyombo vya Habari;**

Tume kupitia vyombo vyenu vya habari ilitangaza ratiba ya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani na kama ambavyo mmesikia, Uchaguzi Mkuu umepangwa kufanyika siku ya Jumatano tarehe 28 Oktoba, 2020. Serikali kwa upande wake tayari imetoa tamko la kuitangaza siku hiyo kuwa ni siku ya mapumziko.

Kwa mujibu wa ratiba hiyo, Fomu za Uteuzi zilianza kutolewa tarehe 5 Agosti, 2020 kwenye Makao Makuu ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Jijini Dodoma kwa wagombea wa Kiti cha Rais. Hadi sasa vyama vya siasa 16, tayari vimechukua fomu hizo. Aidha, Fomu kwa ajili ya wagombea Ubunge na Udiwani zimeanza kutolewa tarehe 12 hadi 25 Agosti, 2020 kwenye Makao Makuu ya Halmashauri yalipo Majimbo na Kata husika.

Aidha, urejeshaji wa fomu utafanyika tarehe 25 Agosti, 2020 kabla ya saa 10 kamili jioni, ambayo ndiyo siku ya uteuzi.

**Ndugu Wahariri wa vyombo vya Habari;**

Kwa mujibu wa ratiba ya uchaguzi, kipindi cha kampeni za uchaguzi kitaanza tarehe 26 Agosti, 2020 hadi tarehe 27 Oktoba, 2020 kwa upande wa Tanzania Bara. Kwa kuzingatia ratiba ya uchaguzi iliyotolewa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) Kampeni za uchaguzi kwa upande wa Tanzania Zanzibar zitaishia tarehe 26 Oktoba 2020 ili kupisha upigaji wa kura ya mapema ya Rais wa Zanzibar, Mwakilishi na Diwani.

Katika kipindi cha kampeni, vyama vya siasa vitapata fursa ya kuwanadi wagombea na kuelezea sera na Ilani za Uchaguzi za vyama vyenu. Katika eneo hili, uzoefu unaonyesha kuwa kipindi cha Kampeni kunakuwa na joto kali la kisiasa linatokana na baadhi ya watu kukosa uvumilivu wa kisiasa hali ambayo inaweza kuhatarisha amani na utulivu wa nchi. Kipindi hicho cha kampeni ndio ambacho vyombo vya habari mnapaswa kuwa makini kwa kuhakikisha kuwa haviwi chanzo cha joto hilo. Njia muafaka ya kuepukana na hilo, ni kuzingatia misingi ya maadili ya kazi yenu.

**Ndugu Wahariri wa vyombo vya Habari;**

Wote tunafahamu kuwa kampeni za uchaguzi zinasimamiwa na maadili ya uchaguzi, hivyo Tume kwa kushirikiana na Vyama vya Siasa pamoja na Serikali tuliandaa Maadili ya Uchaguzi ya mwaka 2020 ambayo yalisainiwa na pande zote mnamo tarehe 27 Mei, 2020. Tume imewapatia vijitabu vya maadili, na ni matarajio yetu kuwa mtavisoma ili kujipatia uelewa.

**Ndugu wahariri wa vyombo vya Habari**;

Maadili hayo ya Uchaguzi, pamoja na mambo mengine, yanavitaka Vyama vya Siasa kufanya Kampeni za kistaarabu na kuepuka kufanya fujo au kuchochea vurugu ya aina yoyote katika mikutano ya vyama vingine; kutokutumia lugha ya matusi, kashfa, kejeli, udhalilishaji na vitisho au lugha inayochochea uvunjifu wa amani au kuashiria ubaguzi wa kijinsia, ulemavu, rangi au maumbile kwenye mikutano na kwenye shughuli zote za kampeni.

Pamoja na shughuli nyingine mnazozifanya, niwaombe kipindi cha kampeni kitumike pia kuwahamasisha wananchi hasa Wapiga Kura kushiriki katika kampeni hizo ili waweze kuwapima wagombea na hatimaye kujitokeza kwa wingi siku ya Kupiga Kura.

**Ndugu Wahariri wa vyombo vya habari;**

Maeneo mengine muhimu kwa wanahabari kuyafahamu ni bajeti ya uchaguzi na vifaa vya uchaguzi. Katika kuandaa na kuendesha Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu, Tume iliandaa Bajeti ya kiasi cha **Tsh. 331,728,258,035.00** zinazotarajiwa kutumika. Kwa kuzingatia kifungu cha 122 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Mfuko Mkuu wa Hazina, itagharimia shughuli zote za Uchaguzi kwa asilimia mia moja.

Katika eneo la vifaa vya uchaguzi Tume inaendelea na mchakato wa ununuzi wa vifaa mbalimbali sambamba na uchapishaji wa fomu, sheria za uchaguzi, kanuni na maelekezo. Jumla ya zabuni ishirini na tano (25) zimetangazwa ambazo zinahusisha uchapishaji wa nyaraka mbalimbali za uchaguzi, na ununuzi wa vifaa vya uchaguzi.

Eneo la Elimu ya Mpiga Kura ni eneo lingine muhimu katika kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi Mkuu. Kwa mujibu kifungu cha 4C cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura ya 343 Tume imepewa mamlaka ya kutoa Elimu ya Mpiga Kura nchi nzima, kuratibu na kusimamia Taasisi au Asasi zenye nia ya kutoa elimu hiyo.

Hivyo, Tume kwa upande wake imejipanga kutoa habari na elimu ya mpiga kura kwa njia mbalimbali ikiwemo matumizi ya Vyombo vya Habari. Katika eneo hili tunategema mchango wenu, Tume inaamimi mtafanya hivyo kwa kuwa mmeshirikiana nasi katika maeneo mengi yaliyotuwezesha kufanikisha majukumu yetu.

Katika kipindi cha uchaguzi Tume itafanya kazi kwa karibu na vyombo vyenu kwa njia mbalimbali ikiwemo kushiriki katika vipindi vya redio na runinga. Baadhi yenu, mmeonesha nia kuanzisha vipindi vinavyohusiana na Uchaguzi Mkuu na mmetuomba tuwe tayari kushiriki mtakapotualika.

**Ndugu Wahariri wa vyombo vya Habari;**
Niwaombe msichoke kuwasisitiza na kuwahimiza wadau na wananchi kwa ujumla kuzingatia Sheria za Uchaguzi, Kanuni na Maelekezo ya Tume. Tume nayo kwa upande wake itaendelea kuzingatia Sheria za Uchaguzi na Kanuni zilizotungwa chini yake katika michakato yote ya uchaguzi.

Aidha, nitoe rai kwenu Wahariri wa Vyombo vya Habari hasa vya umma kutenda haki sawa kwa vyama vyote na kuhakikisha mnawapa wagombea nafasi kutangaza na kunadi sera na ilani za vyama vyao. Aidha, Tume inaanda mafunzo kwa waandishi wa habari watakaohusika na masuala ya uchaguzi ili kuwajengea uwezo wa kuifahamu Tume na majukumu yake na

michakato ya uchaguzi kuanzia Uteuzi, kupiga kura, kuhesabu, kujumlisha kura na kutangaza matokeo.
Ni matarajio ya Tume kuona kwamba vyombo vya habari vinatoa kipaumbele kwa masuala yanayoelekea kujenga umoja wa kitaifa badala ya taarifa na habari ambazo zinachochea vurugu. Tukumbuke kuwa Tanzania sio kisiwa, tusipotumia vizuri taaluma zetu basi kalamu zenu zinaweza kuiingiza nchi kwenye machafuko kama ilivyotokea katika maeneo mengine.

**Ndugu Wahariri wa vyombo vya habari;**
Tume itatoa taarifa kwa wakati kwa kadri itakavyowezekana na inatarajia kuona mkitoa taarifa hizo kwa usahihi, na kwa wakati. Tume inaahidi kuwapa ushirikiano pale mtakapohitaji ufafanuzi wa jambo lolote.
Tume pia itajitahidi kukutana nanyi ili kutoa taarifa juu ya hatua mbalimbali za mchakato wa uchaguzi. Lengo la haya yote ni kuona watanzania wanapata taarifa na wanahamasika ili mwishowe kila mwenye sifa ya kupiga Kura ajitokeze siku ya Uchaguzi.

Tume ina matumaini makubwa ya kufanikisha Uchaguzi huu kwa kutegemea ushiriki wenu katika hatua zote zilizosalia hadi kufikia siku ya uchaguzi. Imani hii inatokana na ushirikiano mlioonesha hususan wakati wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga kura.

Kwa mara nyingine, napenda kuwashukuru tena kwa kuitikia wito na kushiriki kikao hiki muhimu kwetu sote. Tume itaendelea kuwashirikisha kwa kadri itakavyowezekana na kama kawaida itasimamia uchaguzi huu kwa kuzingatia Katiba, Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali zinazosimamia uendeshaji wa uchaguzi. Lengo likiwa ni kuhakikisha Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 unakuwa huru, wa uwazi, wa haki na wa kuaminika kwa kuweka mazingira sawa ya ushindani kwa wagombea na vyama vyote vya siasa vitakavyoshiriki.

***Baada ya kusema hayo, sasa napenda kutamka rasmi kuwa kikao chetu kimefunguliwa.***

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**